JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA AWAMU YA PILI

**AFISA MWANDIKISHAJI, JIMBO LA LUDEWA**

ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA AWAMU YA PILI, UTAFANYIKA KWA SIKU TATU KUANZIA **TAREHE 02/05/2020** HADI **04/05/2020.**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA AWAMU YA PILI UTAFANYIKA KWENYE OFISI ZA KATA TU.**

**WAPIGA KURA WOTE WANATAKIWA KWENDA KUHAKIKI TAARIFA ZAO, KWENYE VITUO WALIVYOJIANDIKISHA.**

**VITUO VITAFUNGULIWA KUANZIA SAA 02:00 ASUBUHI HADI SAA 12:00 JIONI.**

**ZOEZI LA UANDIKISHAJI LITAHUSISHA:**

- ❷ **Kuandikisha wapiga kura wapya waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi na wale watakaotimiza umri huo ifikapo siku ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2020**
- ❷ **Kuandikisha wale wote wenye sifa lakini hawakujiandikisha katika uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura awamu ya kwanza**
- ❷ **Kutoa kadi mpya kwa Wapiga Kura waliopoteza kadi zao**
- ❷ **Kuhamisha taarifa za Wapiga Kura waliohama Kata au Jimbo la Uchaguzi na kuhamia katika eneo jingine**
- ❷ **Kurekebisha taarifa zao Wapiga Kura ambazo zilikosewa**
- ❷ **Kuondoa Wapiga Kura waliopoteza sifa kama vile kufariki.**

**UTARATIBU WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA AWAMU YA PILI:**

- ❷ **Kila Kata kutakuwa na Kituo Kimoja, Mwandishi Msaidizi na BVR KITs ambayo itakuwa na Orodha ya majina ya Vituo vyote vilivyoandikishwa awamu ya kwanza.**
- ❷ **Mpiga Kura yeyote anaweza kuboresha taarifa zake kwa kuzingatia kituo anachotaka kupiga kura siku ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.**

**KUMBUKA:**

**SIFA MUHIMU ZA KUKUWEZESHA KUPIGA KURA SIKU YA UCHAGUZI MKUU MWAKA 2020 NI KUWA NA KADI YA MPIGA KURA!!**

KADI YAKO KURA YAKO, NENDA KAJIANDIKISHE.

**MUHIMU:** *KUMBUKA KUZINGATIA KANUNI ZA AFYA KWA KUFUATA MAELEKEZO UTAKAYOPEWA KITUONI, ILI KUEPUKA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA.*

Gladness Mwano
**KNY: AFISA MWANDIKISHAJI (W)**
**LUDEWA.**

*Tangazo hili linapatikana pia katika tovuti ya Halmashauri: www.ludewadc.go.tz, instagram: ludewa_dc*